

# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1

Fax Nam. + 255 24 2230215

Tovuti: [www.zanzibarassembly.go.tz](http://www.zanzibarassembly.go.tz)



SANDUKU LA BARUA 902,  
ZANZIBAR

Barua Pepe: [zahore@zanlink.com](mailto:zahore@zanlink.com)

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

### **TAARIFA YA SHUGHULI ZA MKUTANO WA KUMI NA MOJA WA BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI UTAKAOANZA TAREHE 19 SEPTEMBER, 2018**

Mkutano wa Kumi na Moja wa Baraza la Tisa la Wawakilishi Zanzibar unatarajiwa kuanza siku ya Jumatano tarehe 19 Septemba, 2018, saa 3:00 asubuhi.

#### **SHUGHULI ZITAKAZOFANYIKA:**

Shughuli za Mkutano huo zitakuwa kama ifuatavyo:-

#### **1. Maswali na Majibu.**

Maswali **154** yameratibiwa kwa ajili ya kujibiwa kwenye Mkutano huu.

#### **2. Miswada ya Sheria**

Miswada ya Sheria iliyowasilishwa na kusomwa kwa mara ya Kwanza katika Mkutano wa mwezi Mei, 2018 itakayojadiliwa katika Mkutano huu wa Kumi na Moja.

Miswada yenyewe ni:-

- i) Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti Bora ya Usimamizi wa Mahakama, Kufafanua Utumishi wa Mahakama, Kuanzisha Ofisi za Mtendaji Mkuu wa Mahakama na Mrajis, Kuanzisha Mfuko wa Mahakama, na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusina na Hayo.
- ii) Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu na Kuweka Masharti ya Ukaguzi wa Elimu Pamoja na Mambo Mengine Yanayohusina na Hayo.
- iii) Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar na kuweka masharti bora yanayohusiana na Kazi, Uwezo, Uongozi na Mambo Mengine Yanayohusina na Hayo.

3. Ripoti za Wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusu utekelezaji wa Maagizo ya Kamati za Kudumu za Baraza kwa mwaka 2017/2018.

**(Raya Issa Msellem)**  
**KATIBU**  
**BARAZA LA WAWAKILISHI**  
**ZANZIBAR**

**Tarehe 17 Septemba, 2018**